



Ujana Tanzania

Ujana Tanzania

Kwa ajili ya vijana wa Tanzania popote walipo

Wewe ni mlingwa wa kitabu hiki kama una miaka kati ya 10 hadi 19.

Lengo la kitabu hiki - Ujana Tanzania: Kwa ajili ya vijana wa Tanzania popote walipo - ni kukuza uelewa na kuchokoza mjadala kuhusu fursa na changamoto zinazowakabili vijana wa Kitanzania kwa wakati huu.

Kisome kitabu hiki, kijadili na walimu wako, wazazi na vijana wenzako, halafu utupe maoni yako. Anuani yetu ni UNICEF, S.L.P 4076, Dar es Salaam au baruapepe daressalaam@unicef.org au unaweza kuwasiliana nasi kwa kupitia Facebook ya UNICEF Tanzania.



Picha za Jalada:

1. UNICEF/Hiroki Gomi
2. UNICEF/Hiroki Gomi
3. UNICEF/Hiroki Gomi
4. UNICEF/Julie Pudlowski
5. UNICEF/Shehzad Noorani
6. UNICEF/Julie Pudlowski
7. UNICEF/Hiroki Gomi
8. UNICEF/Julie Pudlowski

© Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF)

Hairuhusiwi kuiga au kunakili sehemu yoyote ya kitabu hiki bila idhini ya:

Idara ya Mawasiliano na Ushawishi

UNICEF Tanzania

S.L.P 4076

Dar es Salaam

Tanzania

Simu: +255 22 219 6600

Barua pepe: daressalaam@unicef.org

Idhini itatolewa bure kwa taasisi za elimu na mashirika ya hiari.
Wengine wanaweza wakatakiwa kulipia kiasi kidogo cha fedha.

Dar es Salaam, Oktoba 2011



Yaliyomo

| | Kurasa |
|--------------------------------------|---------------|
| 1. Utangulizi | 2 |
| 2. Vijana na Elimu | 7 |
| 3. Tujilinde | 13 |
| 4. Vijana na VVU/UKIMWI | 18 |
| 5. Kuwalinda vijana dhidi ya ukatili | 23 |
| 6. Kuwashirikisha vijana | 28 |
| 7. Vijana wa leo, viongozi wa kesho | 32 |

1



Leila, miaka 10

“Ndoto yangu ni kusaidia kuboresha mfumo wa elimu Tanzania na pia kusaidia watoto yatima kwenda shule.”

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

Utangulizi

Ripoti hii imetayarishwa kwa ajili ya vijana wa Tanzania. Ni muhtasari wa ripoti ndefu kuhusu vijana ambayo iliandikwa kwa ajili ya taasisi za serikali pamoja na viongozi wengine nchini. Ripoti hii inawahimiza viongozi wa umma kuwapa kipaumbele vijana wenye umri kati ya miaka 10 hadi 19. Ripoti pia inawaomba viongozi kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya masuala ya vijana pamoja na kubadilisha sheria kuhakikisha kuwa vijana wanakuwa na fursa nyingi na nzuri kadri wanavyokua.

Si vijana wote nchini Tanzania wanapata fursa ya kwenda shule na kuhitimu. Vijana wengi hawajui jinsi ya kujilinda dhidi ya UKIMWI, wengine ni yatima na wanalazimika kuwatunza wadogo zao. Hali kadhalika, idadi kubwa ya vijana wanafanyiwa vitendo vya ukatili majumbani mwao, shuleni au katika jamii wanazoishi.

Kuna habari njema pia! Tafiti za kitaifa zilifanyika mwaka 2010 kupima maendeleo kuhusu masuala muhimu yanayowahusu vijana. Taarifa nyingi katika ripoti hii zimetoka katika Utafiti wa Demografia na Afya Tanzania (TDHS), ambapo katika utafiti huo familia kote nchini ziliulizwa maswali kuhusu afya, elimu na hali ya maisha. Utafiti wa aina hii hufanywa nchini Tanzania kila baada ya miaka mitano. Tukilinganisha matokeo ya utafiti uliofanywa mwaka 2010 na ule uliofanyika mwaka 2004, tunaweza kuona jinsi mambo yanavyobadilika.

Matokeo ya utafiti wa mwaka 2010 yanaonyesha kuwa wasichana wachache wanaolewa au kupata watoto wakiwa wadogo. Matokeo ya utafiti huo pia yanaonyesha kuwa vijana wengi wanajilinda dhidi ya maambukizi ya VVU.

Vijana wengi wanajihusisha katika shughuli za kuwasaidia kujikimu kimaisha wao pamoja na familia zao—kwa kupitia muziki, elimu rika au kujitolea. Vijana wa leo, wasichana na wavulana, ni viongozi wa kesho: hawa ndio madaktari na manesi, walimu, wasanii, makanika, watengeneza nywele, viongozi wa jamii, wahandisi na watunga sera wa kesho.

Kitabu hiki ni kwa ajili yenu, vijana wa Tanzania. Kinaelezea habari njema na baadhi ya changamoto zinazohitaji ufumbuzi. Tunatumaini kitawasaidia ili muweze kuwa sehemu ya majibu ya changamoto hizo. Kumbukeni hatima ya nchi iko mikononi mwenu.

Ujana ni nini?

Ujana ni kipindi cha mabadiliko makubwa. Hiki ni kipindi ambacho vijana wa kati ya miaka 10 na 19 wanaanza safari ya kuelekea utu uzima. Katika umri wa miaka 10, wengi huwa ni watoto bado. Lakini kwa umri wa miaka 19, baadhi ya waschina na wavulana huwa wameolewa na kuoa, na wengine wanakuwa na watoto tayari. Wengi wao wanafanya kazi ili kupata kipato cha kulisha familia zao. Kwa hiyo miaka hii 10 ni kipindi cha mabadiliko na wakati mwingine ni kipindi cha kuchanganyikiwa. Katika kipindi hiki mabadiliko hutokea katika miili ya vijana, katika hisia zao na namna watu wengine wanavyowachukulia.

Mabadiliko ya mwili hutokea katika nyakati tofauti kwa vijana tofauti, lakini kufikia umri wa miaka 19 wengi wao huwa na maumbile yao ya kiutu uzima.

Katika kipindi hiki vijana wengi wanakuwa na wasiwasi kuhusu mambo mbalimbali—mfano, je, wanavutia? Je, wana marafiki wa kutosha? Na maisha yao yatakuaje hapo baadaye. Wengine wanakuwa na wasiwasi kuwa huenda wameambukizwa VVU au kama wazazi wao watamudu kuwapeleka shule ya sekondari ama kama watakula chakula siku hiyo.

Kipindi cha ujana pia ni kipindi cha uvumbuzi. Ni katika kipindi hiki vijana huiga haiba na tabia mbalimbali na kuona ni tabia zipi zinawafaa zaidi. Katika kipindi hiki cha miaka 10 vijana wengi wanajijengea utambulisho, namna ambavyo wanataka wawe watakapokuwa watu wazima.

Mara nyingi wazazi hutaka vijana wao wachukue majukumu kadri wanavyokua. Baadhi ya wazazi hutaka watoto wao waache shule ili wawatunze wadogo zao au wafanye kazi kwa ajili ya kipato cha familia. Wengine hutaka kuwaoza binti zao wanapofikisha miaka 15 au hata kabla ya hapo.



Fina, miaka 10

“Niliona habari za mauaji ya albino kupitia TV, nikaogopa sana. Najua mama yangu pia aliogopa na kupatwa na mawazo sana akiniwazia mimi. Najisikia salama na amani nikiwa shuleni kwa sababu nipo na rafiki zangu.”

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

Watoto wenye umri wa miaka 10 nchini Tanzania wanaweza kufungwa jela kwa makosa ya jinai. Hii ni kwa sababu sheria inatamka kuwa kwa umri huo ni lazima wawajibike kwa vitendo vyao.

Unaweza kudhani kuwa baadhi ya mambo haya si sahihi. Vijana hutumia muda mwingi kufikiria kipi ni sahihi na kipi si sahihi. Maranyingi huwauliza maswali wazazi wao, walimu na watu wazima wengine. Hii ni sehemu ya kukua na kuamua aina ya mtu wanayotaka kuwa, na ni namna gani wanataka familia na nchi yao iwe. Kuwa na uwezo wa kuongea kwa uwazi kuhusu mawazo yao, hisia na matatizo yao huwasaidia vijana kufikia utu uzima kwa usalama zaidi.

Taarifa na takwimu

- Asilimia 20 ya Watanzania ni vijana. Mmoja katika kila Watanzania watano ni kijana.
- Ni theluthi moja tu ya vijana wanapata fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari
- Takribani nusu ya wasichana wote wenye umri wa miaka 19 wana mimba au tayari wana watoto.
- Wasichana wenye umri wa miaka 18 hadi 19 wana uwezekano mkubwa wa kuambukizwa VVU ikilinganishwa na wale wenye umri wa miaka 15 hadi 17.
- Takribani msichana mmoja kati ya wasichana watatu amedhalilishwa kingono.
- Wavulana na wasichana saba kati ya 10 wamefanyiwa ukatili wa kimwili



Kelvin, miaka 15

“Naipenda shule yangu na ninaifurahia. Hakuna unyanyapaa – wote tunacheza na kufurahi pamoja. Tatizo ni moja tu kwamba siwezi kutumia choo cha shule kwa sababu kina ngazi. Hata hivyo nina bahati kwa sababu ninaishi karibu na shule. Nikitaka kwenda nyumbani siku zote marafiki zangu hunisaidia na kunipeleka na kisha kunirudisha.”

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

Vijana na Elimu

Kupata elimu nzuri ni moja kati ya vitu muhimu ambavyo vijana wa kike na kiume wanapaswa kufanya. Elimu nzuri inawapa nafasi ya kupata kazi nzuri na kupata mshahara mzuri utakaowawezesha kuzitunza familia zao. Vijana waliosoma wanaweza pia kutoa mchango kwa nchi yao kwa kutumia ujuzi na maarifa waliyoyapata katika kutatua matatizo yanayoikabili Tanzania.

Vijana na elimu Tanzania

Miaka michache iliyopita Tanzania ilichukua hatua muhimu kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu ya msingi. Hatua hizo muhimu ni pamoja na kupitisha sheria inayowataka wazazi kuwapeleka watoto wao kupata elimu ya msingi, pamoja na kuondoa ada katika shule za msingi. Hadi kufikia mwaka 2010 asilimia 95 ya watoto wote wenye umri wa kwenda shule walikuwa wameandikishwa.

Baadhi ya shule bado zinawataka wanafunzi kuchangia kiasi kidogo cha fedha, kiasi ambacho baadhi ya familia zinashindwa kukipata. Pamoja na hayo, idadi kubwa ya watoto na vijana (takribani asilimia 20) hawaendi shule au hawamalizi elimu ya msingi. Mikoa ya Shinyanga, Kigoma na Tabora, ambako familia nyingi ni masikini, inaongoza kwa watoto kutomaliza elimu ya msingi. Wakati mwingine wasichana wadogo wenye umri wa miaka 11 au 12 hutolewa shule ili wakaolewe.

Chakula kwa wanafunzi

Mwaka 2007 hadi 2010 Serikali ya Tanzania na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) zilifanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kuwa watoto kutoka maeneo yenye uhaba wa chakula nchini hawashindi na njaa. Chini ya mpango huo watoto 640,000 walipewa chakula shuleni.

Matokeo ya mpango huu yalikuwa mazuri. Mahudhurio ya watoto yaliongezeka katika wilaya ambazo chakula kilikuwa kikitolewa ikilinganishwa na shule nyingine ambazo hazikuwa na mpango huo. Watoto walifanya vizuri darasani, na wengi wao waliendelea na elimu ya sekondari. Idadi ya wanafunzi walioacha shule ilipungua ikilinganishwa na shule za jirani ambazo hazikuwa na mpango wa chakula.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina mpango wa kuanza kutoa chakula katika shule za msingi nchi nzima. Gharama ya chakula kwa mwanafunzi mmoja kwa mwaka ni shilingi 43,500.

Vijana wengi wanaenda sekondari sasa kuliko miaka 10 iliyopita, ingawaje mwaka 2010, vijana wawili kati ya watatu hawakupata nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari.

Wasichana huacha elimu ya sekondari mapema kuliko wavulana. Baadhi ya sababu za hali hii ni kama zifuatazo:

- Wazazi wanawataka wasaidie kazi za nyumbani
- Shule hazina vyoo kwa ajili ya wasichana
- Wasichana wanapata mimba au wanaolewa
- Wasiwasi kwamba mtu anaweza kuwadhuru wawapo shuleni au wakati wa kwenda au kutoka shule.

Hata hivyo, kutokana na umasikini na msukumo wa wazazi wa kutaka vijana wao waanze kufanya kazi mapema kulisha familia, wavulana wengi pia hujikuta wakiacha shule. Hadi kufikia mwaka wa mwisho wa elimu ya sekondari idadi ya wavulana na wasichana wanaosoma huwa sawa—lakini idadi yao wote huwa ni ndogo sana. Ni vijana wanne tu kati ya 100 wanaomaliza miaka sita ya elimu ya sekondari.

Vijana wengi wanashindwa kuendelea na masomo kwa sababu hawafaulu mitihani yao ya mwisho. Wakati mwingine si makosa yao. Shule nyingi hazina vitabu vya kutosha, na kwa hiyo inabidi wanafunzi kadhaa wachangie kitabu kimoja. Majumbani mwao hakuna umeme na hivyo hawawezi kujisomea usiku. Shule nyingi hazina walimu wa kutosha, na kwa maana hiyo madarasa yana wanafunzi wengi kuliko idadi inayotakiwa. Baadhi ya wazazi—hasa wenye kipato cha chini

na wale ambao hawakusoma—hawataki watoto wao wachaguliwe kujiunga na elimu ya sekondari, kwa sababu kama mtoto ataenda sekondari watalazimika kumlipia karo pamoja na mahitaji mengine ya shule.

Kundi lingine ambalo linapata shida ya kukaa shuleni ni kundi la vijana wenye ulemavu. Wengine hawaoni. Wengine hawana mikono au miguu. Shule nyingi hazina miundo mbinu ya kuwasaidia watu kama hawa. Vijana ambao wanatunza ndugu zao wagonjwa, au wao wenyewe wanaumwa, pia hupata wakati mgumu kubaki shuleni. Vijana hawa wenye ulemavu wanapoonewa au kunyanyaswa kwa sababu tu wanaonekana tofauti na wengine wana uwezekano mkubwa wa kuacha shule.

Kwa nini tuwekeze katika elimu?

Elimu ina faida nyingi: (1) faida ya kwanza wanaipata vijana wenyewe kwa sababu wana uwezekano wa kupata maisha mazuri; (2) faida ya pili ni kwa watoto wao na familia zao; na faida ya (3) ni kwa nchi ambayo itanufaika na utaalamu wao.

Kwa mfano: msichana akipata elimu atakuwa na uwezo wa kujitunza vizuri yeye pamoja watoto wake. Wasichana waliosoma pia wanaelewa namna ya kuwalea na kuwatunza watoto, na kwa hiyo watoto wao wana uwezekano mkubwa wa kukua wakiwa na afya. Wasichana waliosoma wana uwezekano mkubwa wa kusubiri mpaka wawe watu wazima kabla ya kuolewa au kushika mimba. Na wavulana na wasichana wanaosoma hujifunza mengi kuhusu UKIMWI na VVU na namna ya kujilinda dhidi ya maambukizi.



Abu, miaka 13

“Tunasoma kitabu kimoja katika wanafunzi wengi, sasa mtu hupati nafasi ya kujisomea mwenyewe. Walimu wamezidiwa sasa sisi wanafunzi tunabidi tujisomee na kujifunza wenyewe. Hivyo ni muhimu kwa kila mwanafunzi kuwa na vitabu vya kujifunzia yeye mwenyewe, kimoja cha Hisabati, Kiingereza na Sayansi.”

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

Njia mbalimbali za kujifunza

Kituo cha Mafunzo ya Ufundi Temeke, Dar es Salaam husaidia zaidi ya vijana 550 kujifunza ujuzi wa kila aina utakaowasaidia kupata kazi. Idadi kubwa ya vijana hawa waliacha shule, lakini bado wanataka kujifunza.



Wanafunzi wanaweza kujifunza kuhusu umeme, mapishi, useremala, ushonaji, utengenezaji batiki, chakula bora, sanaa na utengenezaji nguo. Wanafunzi walio katika kituo hiki wanaishi na wazazi au jamaa zao. Vijana wengi wanaosoma kwenye kituo hiki wanakumbana na vikwazo vingi. Kituo kinawafudisha vijana stadi za maisha kila Ijumaa na kuwahimiza kushiriki kwenye baraza la shule ambapo hujifunza namna ya kujieleza na kujiandaa kwa maisha baada ya kumaliza mafunzo.

Picha: UNICEF/Julie Pudlowski

Tafakari

Kama serikali ingetenga fedha nyingi kwa ajili ya elimu; fedha hizo zingetumika kusomesha walimu wengi, kununulia vitabu na kuifanya elimu kuwa rahisi ili kila mzazi aweze kumpeleka mtoto wake sekondari.

Unadhani fedha kwa ajili ya elimu ingetumikaje zaidi?

Nini maoni yako?

Tuandikie: UNICEF, S.L.P 4076, Dar es Salaam
au baruapepe daressalaam@unicef.org

3



Elizabeth, miaka 18

*akipima malaria katika
Kilini ya Yombo Vituka
mjini Dar es Salaam
inayotoa Huduma Rafiki za
Afya kwa Vijana.*

*Vijana wanaojitolea katika
kliniki hiyo hujulikana
kama 'Waelimishaji Rika,'
huwafundisha vijana
kuhusu hatari ya vitendo
vya ngono zembe; VVU;
mimba na ndoa za utotoni;
matumizi ya dawa za
kulevya na pombe.*

*Pia huwafundisha kuhusu madhara ya biashara ya ukahaba, ukatili
na unyanyasaji.*

*Hassani ni miongoni mwa vijana wanaojitolea. Anaeleza,
"Wasichana wadogo hupenda kuja katika huduma rafiki za afya kwa
sababu wanajisikia huru, wana faragha na wanaweza kuzungumza
kwa uwazi. Wakienda kwenye kliniki za kawaida, wanaweza
kukutana na jirani zao na marafiki au madaktari ambao si rafiki
kwa vijana hivyo wanashindwa kueleza matatizo yao halisi. Kupitia
huduma rafiki ya afya vijana wanapata elimu kuhusu kujamiiana na
afya ya uzazi, pia wanapata msaada waelimishaji rika."*

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

Tujitunze

Watoto wachanga na watoto wadogo wanakumbana na hatari nyingi za kiafya na uwezekano wa kuishi. Vijana nao wana matatizo yao mengi, kama:

1. Kuolewa wakiwa wadogo na kupata watoto (kwa wasichana)
2. Kutokupata chakula kizuri na cha kutosha
3. Kumpata mtaalamu wa afya au daktari ambaye anaweza kuwaelewa vizuri

Ndoa za utotoni, mimba na uzazi

Mabadiliko makubwa yalitokea nchini kati ya mwaka 2004 na 2010 miongoni mwa wasichana wenye umri kati ya miaka 15 na 19. Mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo:

- Idadi ya ndoa kati ya wasichana na watu wazima zilipungua kwa asilimia 25
- Mimba na uzazi vilipungua kwa asilimia 12, hasa miongoni mwa wasichana wenye umri mkubwa
- Matumizi ya njia za kuzuia mimba yaliongezeka mara mbili, kutoka asilimia 8 hadi asilimia 16

Hii ni habari njema kwa wasichana kwa sababu wengi wao huwa hawapendi kuolewa wakiwa wadogo, bali hushinikizwa na waume au familia zao. Wakishaolewa hutegemewa na waume na familia zao wazae watoto.

Viungo vya wasichana wadogo bado havijawa tayari kubeba mimba na hivyo wanakuwa katika hatari kubwa ya kupoteza maisha au kupata vilemavyamaishawakati wakujifungua. Kamamsichana mwenyemimba hatapata chakula cha kutosha, au hatapata chakula chenye virutubisho, yeye na mtoto wake wanaweza kuathirika kiafya na hata kupoteza

maisha kutokana na utapiamlo. Uwezekano wa msichana mwenye umri mdogo kumhudumia vizuri mtoto wake ni mdogo, na pia mtoto aliyezaliwa na mama mwenye umri mdogo ana uwezekano mkubwa wa kufariki katika mwezi wa kwanza tangu kuzaliwa ikilinganishwa na mtoto aliyezaliwa na mama mwenye umri mkubwa.

Wasichana wanaopata mimba hufukuzwa shule. Sheria inasema kuwa wasichana waliopata mimba waruhusiwe kurudi shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua. Lakini baada ya kuzaa inakuwa vigumu sana kwa msichana kurudi shuleni kwa sababu, kwanza, ni lazima atafute mtu wa kukaa na mtoto wake wakati yeye anapokwenda shule, pili, anaogopa kuchekwa na kunyanyapaliwa na wanafunzi wenzake, na tatu, anaweza kufanyiwa udhalilishaji wa kingono.

Kwa hiyo ukweli kwamba wasichana wengi wanajaribu kuzuia mimba, na kuolewa baada ya kuwa na umri mkubwa, ni kielelezo tosha kuwa wasichana wa Tanzania ni weledi na wanajitunza. Hata hivyo, wasichana wengi wanatakiwa kufuata mfano huu.

Chakula cha kutosha na mlo sahihi

Kupata chakula cha kutosha, na kula chakula ambacho mwili unahitaji kwa ajili ya kukua ni tatizo kubwa kwa vijana. Familia masikini hazina chakula cha kutosha. Katika familia kubwa inaweza kuwa vigumu kumpatia kila mwanafamilia chakula cha kutosha. Katika familia nyingine wanaume na vijana wa kiume hupewa chakula kizuri na chenye virutubisho kama vile nyama, huku wanawake na vijana wa kike wakila vyakula visivyo na virutubisho vya kutosha.

Miili ya vijana inakua kwa haraka sana, na kwa maana hiyo wanahitaji kupata chakula cha kutosha. Kama hawatapata vyakula vyenye virutubisho vya kutosha wanaweza kupata tatizo la upungufu wa damu. Hii ina maana kuwa miili yao haina virutubisho vinavyohitajika, hasa madini ya chuma, ili iweze kukua na kujijenga.

Wakikosa virutubisho hivyo watajisikia dhaifu na kuchoka na wanaweza kushambuliwa na magonjwa mara kwa mara. Wasichana na wavulana wasiopata chakula cha kutosha au chakula chenye virutubisho muhimu hawawezi kufanya vizuri katika masomo yao. Vijana wa kike wana uwezekano mkubwa (zaidi ya mara mbili) wa kupata tatizo la ukosefu wa damu kuliko wavulana. Utafiti uliofanywa hapa nchini ulionyesha kuwa asilimia 75 ya wasichana walikuwa na tatizo la ukosefu wa damu katika mimba zao za kwanza.

Utafiti mwingine ulifanyika Tanga kuona kama kutakuwa na mabadiliko yoyote kwa wasichana wajawazito iwapo watapeva vidonge vya madini ya chuma kila wiki. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa wasichana waliopata madini ya chuma walikuwa na uwezekano mdogo wa kupata tatizo la ukosefu wa damu, na watoto wao walikuwa na afya nzuri zaidi. Watu wengi hawaelewi kuwa kutumia chumvi yenye madini joto inawasaidia watoto kukua vizuri na kufanya vizuri katika masomo yao.

Kula matunda na mboga nyingi husaidia miili ya vijana wa kike na kiume kupambana na maradhi.

Huduma rafiki ya afya kwa vijana

Moja ya sababu kubwa inayowafanya vijana wasiende hospitali au vituo vya afya wanapoumwa (au kupima VVU au magonjwa mengine ya ngono) ni woga wa kuonekana kwenye vituo vya afya ambapo upimaji unafanyika. Wanajisikia aibu. Wanakuwa na wasiwasi kuwa wazazi wao watajua kuwa wameanza kufanya ngono —au kwamba madaktari na manesi hawawezi kuwafichia siri, au watawakaripia. Serikali imeanzisha huduma za afya rafiki kwa vijana ili waweze kupata huduma waitakayo bila woga.

Takribani theluthi moja ya vituo vya afya nchini vina huduma rafiki kwa vijana, kwa ajili ya upimaji wa VVU, vidonge vya kuzuia mimba na matibabu ya magonjwa ya ngono.

Tafakari

Kama serikali ingetenga fedha za kutosha kusaidia vijana wawe na afya nzuri; itoe vidonge vya madini ya chuma kwa wasichana wajawazito ili kuzuia tatizo la ukosefu wa damu. Ingewaelimisha Watanzania wote kuhusu madhara ya wasichana wadogo kuolewa na kuzaa katika umri mdogo. Serikali pia ingesaidia kuanzishwa vituo vingi vya afya vinavyotoa huduma rafiki kwa vijana.

Unadhani nini kingine kinatakiwa kufanyika? Fedha hizo za serikali zitumike namna gani? Nini mawazo yako?

Tuandikie: UNICEF, S.L.P 4076, Dar es Salaam
au baruapepe daressalaam@unicef.org

4



Sharifa, miaka 11, anaeleza kuwa:

"Baba yangu alikufa kwa UKIMWI, wakati nilipokuwa bado mdogo, hata kabla sijaanza shule. Kila nikimkumbuka natamani kulia kwa sababu sina tena baba si kama watoto wengine. Nilikuwa na miaka 10, ndipo nilipogundua kwamba pia nina VVU... mama yangu aliniketisha chini na kunieleza kuwa ni kweli kwamba nina VVU.

Nililia sana, mama alijaribu kunifaraji. Shuleni watoto wenzangu huambizana 'msikae nae au kuongea nae kwa sababu ana VVU.'

Ninahuzunika wanaposema maneno hayo. Ninapokuwa nyumbani napenda kula chakula nje ya nyumba, lakini akinamama wengine humwambia mama yangu asiniruhusu kula nikiwa nje ya nyumba kwa sababu wanaogopa nitawaambukiza watoto wao VVU kama nikila nao chakula. Nikaacha kula chakula nje ya nyumba. Nataka kuwaambia watoto wengine wasinitenge kwa sababu ya hali yangu. Mcheze nami, mle nami na twende shule pamoja. Hii itanipa furaha na amani."

Picha: UNICEF/Sala Lewis

Vijana na VVU/UKIMWI

Takribani vijana wote nchini wameshasikia kuhusu virusi vinavyosababisha maradhi ya UKIMWI (VVU) na UKIMWI, ingawaje ni nusu tu ndio wanajua namna watu wanavyoambukizwa ugonjwa huu hatari. Kama hilo hawalijui, basi ni dhahiri kuwa hata wao wenyewe hawajui wanavyoweza kujikinga

VVU vina ambukizwa kwa njia mbalimbali, vinaweza kutibiwa (lakini sio kupona) kwa kutumia mchanganyiko wa dawa maalumu inayoitwa 'anti-retrovirals,' au ARVs. UKIMWI ni ugonjwa ambao watu hupata kama wana VVU lakini hawapati matibabu.

Ingawa njia kubwa ya maambukizi ya VVU ni kwa kupitia ngono, kuna njia nyingine za kupata virusi hivyo. Mama mwenye VVU au UKIMWI anaweza kumwambukiza mtoto wake wakati wa kujifungua au wakati wa kumnyonyesha.

VVU pia vinaweza kuambukizwa kwa kuchangia sindano na mtu mwenye maambukizi au wakati wa kutoga masikio. Vinaweza kusambaa pia kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali (kama kisu, wembe au sindano) ambacho kina damu yenye maambukizi. Wasichana wanaokeketwa na wavulana wanaotahiriwa kienyeji wana hatari ya kuambukizwa VVU kwa sababu kisu kimoja kinatumika kwa watu wengi. Ubakaji pia unaweza kusababisha kuambukizwa VVU endapo mbakaji ana virusi hivyo.

Watu wengi wenye virusi, hasa watoto na vijana, wameambukizwa bila ridhaa yao. Lakini ni bahati mbaya kuwa baadhi ya watu hawalielewi hili, na wakati mwingine wanakuwa wakatili kwa watu wenye VVU na UKIMWI.

VVU haviambukizwi kwakula au kushikana mikono au hata kukumbatiana na mtu mwenye ugonjwa huo.

Wakati mwingine vijana hujilingizakatika vitendo vinavyoweza kuwaweka katika hatari ya kuambukizwa VVU. Mfano kuwa na wapenzi wengi; au kufanya ngono bila kondomu; au kufanya biashara ya ngono ili kupata fedha, chakula au nguo.

Vijana wengi wanafikiria 'haiwezi kutokea kwangu'. Au hawajui kuwa unaweza kuambukizwa VVU kwa kufanya ngono mara moja tu!

Inakadiriwa kuwa watoto na vijana 160,000 chini ya miaka 15 wanaishi na VVU nchini. Ni nusu tu ya idadi hiyo wanatibiwa kwa ARVs. Takribani wasichana na wavulana 30,000 wenye umri kati ya miaka 15 na 17 wanaishi na VVU. Hata hivyo wanapofika umri wa miaka 18 na 19 zaidi ya maradufu ya idadi hiyo huwa wameambukizwa VVU.

Vijana wanapoanza ngono mapema uwezekano wa kuwa na wapenzi wengi ni mkubwa, na pia wanakuwa na hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa VVU.

Dalili njema

Vijana wengi siku hizi wanapima VVU. Asilimia 7 tu ya vijana walipima UKIMWI mwaka 2004, ikilinganishwa na mwaka 2010 ambapo asilimia 35 ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 19 walipima. Hii ni dalili njema kwa sababu watakaogundulika kuwa wameathirika watapewa dawa na kuepuka kuwaambukiza wengine. Idadi ya wavulana wanaopima VVU imeongezeka, ingawaje ni asilimia 15 tu. Ni muhimu kwa vijana wengine wasichana na wavulana kupima VVU.

Ili kuhakikisha kuwa wao na watoto wao hawaathiriki na VVU, vijana wanahitaji kujifunza zaidi kuhusu VVU na namna ya kuzuia maambukizi yake. Vijana wanahitaji kujifunza kutoka kwa wazazi, walimu, madaktari na manesi, viongozi wa dini, vikundi vya vijana na vyanzo vingine. Vijana wenye elimu ya msingi na hasa kutoka



Abasi, miaka 15, alisema:

Nakumbuka vema siku ambayo mama yangu aliniambia kwamba ana VVU, sikumuamini. Nilikuwa na umri wa miaka 11, nikaenda kumuuliza baba yangu, akaniambia ni kweli. Nilikwenda ufukweni nikatembea peke yangu kwa muda mrefu nikijiuliza mama yangu amepataje VVU. Baadaye nikaamua kwamba nitamtunza mama yangu ili naye aendelee kunitunza. Nilijiunga na ZAPHA+, ni taasisi inayosaidia familia zilizoathirika na UKIMWI.

Naipenda klabu yangu ya ZAPHA+ kwa sababu inaniwezesha kuwa na watoto wengine ambao pia wameathirika kwa UKIMWI na tunacheza na kufurahi pamoja. Kila Jumapili, mimi na mama tunaketi na watoto na tunawafundisha kuhusu VVU na UKIMWI na jinsi ya kuishi kwa amani kati yetu. Kuwatenga watu wanaoishi na VVU na UKIMWI si jambo jema. Mama yangu ni mfanyakazi wa idara ya afya, anaishi na VVU, lakini ananitia moyo.

Picha: UNICEF/Sala Lewis

familia duni nchini wana uelewa mdogo kuhusu namna ya kuzuia maambukizi ya VVU ikilinganishwa na vijana waliofika elimu ya sekondari au wanaotoka katika familia zenye kipato kikubwa.

Jamii pia inatakiwa kujifunza kuwapenda watu wanaoishi na VVU na sio kuwalaumu au kuwafanya wajisikie wakiwa. Asasi isiyo ya kiserikali inayoitwa Chama cha Watu Wanaoishi na virusi vinavyosababisha maradhi ya UKIMWI na UKIMWI Zanzibar (ZAPHA+) inawasaidia watu kujifunza kutowanyapaa waathirika.

Tafakari

Kamaserikali ingetengafedhazakutoshakwaajiliyavijana ingehakikisha kuwa vijana wengi wanaelimishwa kuhusu VVU na namna ya kujilinda dhidi ya maambukizi. Ingesaidia pia mipango mingi kama ya ZAPHA+ kusaidia watu wanaoishi na VVU na familia zao na kupiga vita unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na VVU.

Unadhani nini kingine kifanyike? Nini maoni yako?

Tuandikie: UNICEF, S.L.P 4076, Dar es Salaam
au baruapepe daressalaam@unicef.org



Simulizi ya Penina

Penina alikuwa na umri wa miaka 11 wakati kijana mwenye umri wa miaka 19 alipomtaka amuo. Rafiki zake walimshauri kukubali mpango huo wakimweleza kuwa atakuwa na maisha mazuri. Akiwa mkubwa kati ya watoto sita kwenye familia, maisha yalikuwa magumu hivyo alikubali kuolewa.

“Miezi miwili baada ya kufunga ndoa mume wangu alianza kunipiga,” alisema.

Baada ya kujifungua mtoto wa kwanza, mumewe alimtuhumu kuwa na uhusiano na mwanaume mwingine na kwamba mtoto huyo si wake. “Alisema ataniua na kunizika mimi na mtoto wangu. Alianza kunipiga sehemu mbalimbali za mwili kwa mpini wa shoka.”

“Mama mkwe wangu alisikia nikipiga kelele na kuja kuniokoa. Baba yangu alikuja na kumwambia mume wangu aache kunipiga, lakini ikawa mbya zaidi. Alinipiga zaidi ya awali.”

Mwishoni Penina alichukuliwa na mama yake kwa ajili ya usalama. Alirudi nyumbani na uongozi wa mtaa ulivunja ndoa hiyo. Hivi sasa ana umri wa miaka 13 na watoto wawili wadogo. Matamaini yake makubwa ni kurudi shuleni.

UNICEF/Hiroki Gomi

Kuwalinda vijana dhidi ya ukatili

Ni jukumu la serikali kuwalinda watoto na vijana dhidi ya ukatili wa aina yoyote kwa mujibu wa sheria za nchi na mikataba mbalimbali ya kimataifa. Kwa mfano, serikali ilitia saini Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki ya Mtoto na Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto. Mwaka 2009 Bunge lilipitisha Sheria ya Mtoto. Mwaka 2011, Baraza la Wawakilishi Zanzibar nalo lilipitisha Sheria ya Watoto.

Sheria hizi pamoja na mikataba zinasema kuwa watoto na vijana wana haki, ikiwemo haki ya kulindwa dhidi ya ukatili wa aina yoyote.

Wazazi, familia, walimu, polisi na jamii nzima wana jukumu la kuwalinda watoto. Lakini hata hivyo jambo la kusikitisha ni kwamba wakati mwigine watu wanaotakiwa kuwalinda watoto wanashiriki kuwafanyia ukatili. Kwa mfano: nchini Tanzania ni halali kisheria kutoa adhabu ya viboko kwa vijana, iwe shuleni au majumbani. Baadhi ya wazazi huamini kuwa viboko vitawafanya watoto wawe na adabu. Hata hivyo ukweli ni kwamba viboko havisaidii, na ni ukiukaji wa haki ya mtoto ambayo inatakiwa kulindwa.

Matokeo ya utafiti kuhusu ukatili dhidi ya watoto nchini yalitolewa mwaka 2011. Watafiti walihoji maelfu ya vijana wenye umri kati ya miaka 13 hadi 24 kama walifanyiwa ukatili wakati wanakua. Utafiti ulionyesha yafuatayo:

- Takribani wasichana watatu kati ya 10 na mvulana 1 kati ya 7 walifanyiwa ukatili wa kingono kabla ya kufikia umri wa miaka 18
- Asilimia 6 ya wasichana walilazimishwa kufanya ngono kabla ya kufikia umri wa miaka 18
- Wapenzi, majirani, na wageni ndio wahusika wakuu wa ukatili wa kingono dhidi ya wasichana na wavulana

- Vitendo hivyo vya ukatili wa kingono mara nyingi vilifanyikia katika nyumba ya mtu au wakati wa kwenda shule
- Vitendo vingi vilifanyika wakati wa mchana

Utafiti pia ulionyesha kuwa robo ya wasichana na wavulana walifanyiwa ukatili wa kuumiza hisia kwa kutishiwa kutelekezwa au kwa kufanyiwa vitendo vilivyowafanya wajione kama watu wasiotakiwa katika jamii.

Nini kifanyike

Tanzania sasa imeanzisha chombo cha Serikali, Kikosi Kazi cha Sekta Mbalimbali kinachoshughulikia Ukatili Dhidi ya Watoto, ambacho kimepanga kufanya yafuatayo:

1. Kutoa mafunzo kwa jamii, polisi, madaktari, walimu na wafanyakazi wa ustawi wa jamii kuhusu namna ya kutoa msaada kwa vijana wanapopata matatizo, na
2. Kuelimisha jamii namna ya kuwalinda watoto dhidi ya aina yoyote ya udhalilishaji na ukatili

Kikosi Kazi hicho kitahakikisha kuwa haki za mtoto kama zilivyoanishwakwenye Sheri ya Mtoto ya mwaka 2009 zinalindwa. Hata hivyo zoezi hili linahitaji fedha nyingi wakati ambapo serikali ina mahitaji mengi.

Pamoja na kwamba idadi ya vijana wanaoolewa katika umri mdogo imepungua, bado msichana mmoja kati ya wasichana sita anaolewa kabla ya kufikia umri wa miaka 19. Baadhi ya wasichana wanaoolewa katika umri mdogo baadaye hujutia uamzi wao kutokana na mateso wanayoyapata katika ndoa zao. Wasichana wengi wanaoolewa katika umri mdogo wanakatazwa na waume zao kutembelea familia zao, au marafiki zao au kwenda shule. Pia hawana uhuru wa kuamua kuzaa au kutozaa, au kufanya uamuzi wowote kuhusu maisha yao.



Watoto wanaoishi mitaani mara nyingi huondoka nyumbani kwao kwa sababu ya mateso, unyanyasaji na njaa.

“Kwa kidogo tulichonacho, tunasaidiana,” alisema msichana mmoja anayeishi mitaani mkoani Mwanza.

Picha: UNICEF/Shehzad Noorani

Takribani msichana mmoja kati ya wasichana watatu walioolewa anasema alisukumwa, alitingishwa, alipigwa makofi, mateke, ngumi, alichomwa moto, alitishiwa au alishambuliwa kwa kisu au bunduki na mume wake.

Maisha ya mitaani

Wakati mwingine watoto na vijana hukimbia majumbani mwao na kwenda kuishi mitaani kutokana na ugumu wa maisha katika familia zao. Wengine hukimbia baada ya kukosa chakula cha kutosha katika familia zao kutokana na umasikini, wengine hukimbilia mitaani baada ya wazazi

wao kufariki dunia kutokana na ugonjwa wa UKIMWI au wanakimbia nyumbani kukwepa vipigo.

Wanapofika mitaani wanakumbana na maisha magumu sana, maisha ya kulala kwenye maboksi, tena kwenye baridi. Watoto wa mitaani wenye umri mkubwa kuliko wao huwaibia na kuwapiga. Wakati mwingine polisi huwakamatanakuwawekandani. Wote, wasichana wawulana, wanakuwa katika hatari ya kubakwa au kudhalilishwa kingono. Watoto wa mitaani wanapata shida ya kutafuta fedha ya kula na ya kuwawezesha kuishi, na wengi wao hawaendi shule. Nchini Tanzania na katika nchi nyingi duniani, watoto wanaoishi mitaani ni wale wanaotoka katika familia duni.

Watoto wa mitaani pia wanaweza kutekwa na kulazimishwa kufanya kazi za hatari. Wakati mwingine kazi wanazolazimishwa kufanya ni ngumu na za hatari kwa afya zao. Wawulana na wasichana pia wanaweza kutumika katika ukahaba. Mara nyingi wale wanaowachukua kufanya kazi hizo huwaahidi kuwa watawatafutia kazi nzuri na kuwapeleka shule, ahadi ambazo mara nyingi si za kweli.

Familia zinatakiwa kujua namna ya kuwalinda vijana na watoto dhidi ya aina yoyote ya ukatili. Madaktari wanatakiwa kujifunza namna ya kuwahudumia vijana ambao wamedhalilishwa kingono. Vijana wanaotaka kutoa ripoti ya uhalifu ni lazima walindwe na polisi na taarifa zao zichukuliwe kwa faragha, na watoto wasichanganywe na watu wazima katika mahabusu au jela.

Tafakari

Ni namna gani unadhani vijana wanaweza kulindwa dhidi ya ukatili? Kikosi Kazi kichukue hatua gani kulinda vijana dhidi ya ukatili wa kingono? Nini maoni yako?

Tuandikie: UNICEF, S.L.P 4076, Dar es Salaam
au baruapepe daressalaam@unicef.org



Venancia ajitolea na Ishi

Alipokuwa katika kidato cha kwanza, Venancia alishinda tuzo ya utunzi wa nyimbo uliodhaminiwa na Ishi, Kikundi cha Tanzanian kinachojihusisha na kuwakinga vijana na VVU.

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

Kuwashirikisha vijana

Sheria ya Mtoto Tanzania inasema hivi: “Mtoto ana haki ya kuelezea mawazo yake, kusikilizwa na kushiriki katika maamuzi yanayohusu maisha na ustawi wake.”

Vijana wanapopata fursa ya kuzungumza kuhusu maamuzi yanayofanywa na familia zao, shuleni kwao au katika jamii zao, huwafundisha namna ya kujieleza, namna ya kuwasikiliza wengine na kuheshimu mawazo tofauti. Vijana hujifunza namna ya kuomba kile wakitakacho, na wanajifunza kuwa

wakati mwingine inawabidi wakubali kile watu wengine wanachokitaka. Hili ni fundisho muhimu katika maisha.

Kwa bahati mbaya, nchini Tanzania vijana hawashirikishwi. Katika familia nyingi vijana huambiwa nini cha kufanya na hupewa adhabu wakikataa kutii.

Shule nyingi haziwaulizi wanafunzi kuhusu maoni yao. Baadhi ya shule Tanzania zina mabaraza ya wanafunzi (makundi ya wanafunzi yaliyochaguliwa kuwakilisha madarasa yao). Tafiti zimeonyesha kuwa shule zenye mabaraza ya wanafunzi hazina migogoro na hufanya vizuri katika mitihani ya mwisho. Walimu na wanafunzi pia hushirikiana vizuri katika shule za aina hii.

Hata hivyo fursa za kushiriki zipo, na vijana wengi sasa wanashirikishwa.

Baraza la Watoto ni njia nyingine ya kuwawezesha vijana kushiriki. Baraza la kwanza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilianzishwa mwaka 2002. Hivi sasa vijana wanaweza kujiunga na mabaraza madogo katika wilaya 90 nchi nzima.

Wajumbe wa Baraza la Watoto wa Tanzania Bara na Zanzibar wamekutana na maofisa wa serikali za mitaa kutoa maoni yao kuhusu masuala kama: adhabu za viboko, sheria ya ndoa, huduma za afya na kulinda haki za vijana.

Roots and Shoots

Njia nyingine ambayo inaweza kuwasaidia vijana kushiriki katika dunia inayowazunguka ni kujitolea kufanya mambo ambayo wanayapenda. Wale ambao wanapenda kutunza mazingira mara nyingi hufanya kazi na 'Roots and Shoots,' ambayo ilianzishwa takribani miaka 20 iliyopita, na ambayo sasa inafanya kazi katika shule nyingi kote nchini.



Mayasa, miaka 17, kutoka Zanzibar

Ni mwanachama wa Mtandao wa Wanahabari Watoto Tanzania.

“Nilifurahi sana kushika rekoda kwa mara ya kwanza na kujifunza jinsi ya kuitumia.”

Vipindi vya redio vilivyoandaliwa na Mayasa na vijana wengine kutoka Mtandao wa Wanahabari Watoto Tanzania vinaweza kusikilizwa kila wiki kupitia kipindi cha ‘Toto’s Corner’ katika Zenji FM 96.8 FM kila Jumapili saa nne asubuhi. ‘Mlango wa Watoto’ kupitia masafa ya 92.2 FM, Redio Sauti ya Injili kila Jumapili saa nane mchana, pia kupitia ‘Paza Sauti’ katika Redio Tumaini na kupitia ‘Wasaa Wetu’ katika Pambazuko FM kila Jumamosi asubuhi.

Picha: UNICEF/Jacqueline Namfua

Kupitia Roots and Shoots, vijana wanatoa mchango wao katika kuboresha mazingira kwa kushiriki katika kampeni za upandaji miti, kusafisha makazi, kutunza wanyama pamoja na shughuli nyingine kama hizo.

Si rahisi kwa vijana kujua fursa zilizopo ili waweze kushiriki. Ni vigumu sana kupata habari kama hawana Mtandao, luninga au gazeti, au hawasomi shule. Vijana wengi nchini wanategemea redio kupata taarifa. Wale wanaoishi mijini wanapata habari kupitia vyombo mbalimbali vya habari, hata hivyo hakuna vipindi vingi vinavyowahusu vijana katika vyombo hivyo vya habari.

Vipindi vya redio vinavyoandaliwa na Mtandao wa Wanahabari Watoto, ni moja ya vipindi ambavyo vinatoa fursa kwa vijana. Vijana wanashiriki kuviandaa na kuvitangaza vipindi hivyo. Hali kadhalika kipindi cha Mtoto kwa Mtoto kinachorushwa na Radio Kwizera pia kina manufaa makubwa kwa watoto wanaoishi nchini kama wakimbizi kutoka nchi nyingine.

Tafakari

Kama ungekuwa na kipindi cha redio, ungeongelea kuhusu nini? Je, kituo cha redio yako ya jamii kina vipindi ambavyo vinawapa vijana fursa ya kujadili masuala yanayowahusu? Tuambie ni kwa njia gani unachangia jamii na shule yako.

Tuandikie: UNICEF, S.L.P 4076, Dar es Salaam
au baruapepe daressalaam@unicef.org



Rachel, miaka 19

*"Mimi ninaimba kuhusu
ninachokiona katika jamii.
Ninaimba kuhusu kilicho cha
kweli."*

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

Vijana wa leo, viongozi wa kesho

Baada ya miaka 10, vijana ambao wana miaka 15 leo watakuwa na umri wa miaka 25. Labda utakuwa na familia yako na kazi au taaluma fulani. Utakuwa kizazi kipya kinachofanya maamuzi muhimu na kusaidia kujenga nchi.

Takwimu zilizobainishwa hapo awali zinaonyesha kuwa vijana wengi hawatakuwa tayari kubeba majukumu haya. Tumeona kuwa kumekuwa na maendeleo, lakini bado maendeleo zaidi yanahitajika.

Mambo yafuatayo lazima yafanyike ili kuhakikisha kuwa kizazi kijacho cha Tanzania kinakuwa cha watu wenye afya na ambao wamejiandaa vyema kuchukua jukumu la kuliendeleza taifa:

- Vijana wengi wanamaliza shule ya msingi na sekondari
- Wasichana wachache wanaolewa katika umri mdogo, ili waweze kumaliza shule, kutoa maamuzi sahihi kuhusu afya zao na kuwa na watoto wenye afya
- Vijana wengi wanapata taarifa sahihi kuhusu namna ya kuzuia maambukizi ya VVU
- Vijana (hasa wasichana) wanalindwa dhidi ya vitendo vyovyote vya kikatili dhidi yao
- Vijana wanapewa nafasi ya kuchangia mawazo kuhusu maamuzi yanayogusa maisha na maslahi yao, iwe ni shuleni au katika jamii wanazoishi.

Viongozi wa kitaifa wamekuwa wakichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa mambo haya yanafanyika. Kwa mfano: Serikali iliondoa ada ya shule za msingi ili hata watoto kutoka familia masikini waweze kupata elimu. Serikali ilipitisha Sheria ya Mtoto, imeanzisha vituo vinavyojali afya kwa vijana, na imeunda Kikosi Kazi kwa ajili ya kushughulikia ukatili dhidi ya watoto.

Lakini si kila tatizo linaweza kutatuliwa na sheria pekee. Ili kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kwa mfano, kila mtu lazima akubali kuwa ukatili na udhalilishaji ni kosa. Ili wazazi waweze kushawishika kuwapeleka watoto wao shule ni lazima ihakikishwe kwamba wazazi wote wanaelewa umuhimu wa elimu kwa vijana wa leo. Kwa maneno mengine, ili kutatua baadhi ya matatizo ni muhimu kubadilisha tabia za watu wote.

Vijana wanaweza kusaidia kusambaza taarifa hizi. Vijana wa leo wanaweza kusaidia kuleta mabadiliko kwa kufikisha ujumbe wa mabadiliko kwa rafiki zao, wanafunzi wenzao na familia zao, na kwa kujenga tabia ya kujali afya zao. Unaweza kuwa mfano—kama mwelimishaji rika, mtu anayejitolea,



Wasichana hawa wakicheka wakati mchezo wa kuigiza kuhusu VVU na UKIMWI. Burudani ikitumiwa inaweza kusaidia kufikisha ujumbe popote walipo vijana.

Picha: UNICEF/Julie Pudlowski

mjumbe wa Baraza la Watoto – kwa ajili ya kusaidia vijana wengine. Unaweza kuamua unachoona ni sahihi au si sahihi, na ujaribu kusimamia ukweli, kupitia nyimbo, michezo ya kuigiza, vipindi vya redio vya vijana na mabaraza ya wanafunzi.

Tunatumaini kuwa kila kijana anayesoma kitabu hiki atajifunza kitu kipya. Na tunatumaini kitabu hiki kitakusaidia kujiandaa kupambana na majukumu yanayokusubiri.

Tuandikie: UNICEF, S.L.P 4076, Dar es Salaam
au baruapepe daressalaam@unicef.org